TAMADUNI ZA IMANI ZA ULIMWENGU

MAJIBU YA MAJARIBIO

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Somo la 3
Umomoni

(1) Wamomoni wanaamini nini kuhusiana na Ukristo wa Kihistoria?

Ukristo wa kweli uliisha na vifo vya mitume na haukuwepo tena hadi Smith alipoanzisha kanisa la Momoni.

(2) Lengo kuu la Wamomoni ni nini?

Kuwa mungu baada ya kifo.

(3) Wamomoni wanaamini nini kuhusu Yesu kabla hajazaliwa?

Alikuwa roho, kama malaika wengine; hakuwa Mungu.

(4) Wamomoni wanafikiri nini kuhusiana na makanisa mengine?

Makanisa mengine yote ni ya kishetani.

(5) Mamlaka ya juu ya Wamomoni ni nini?

Ufunuo wa Joseph Smith.

Somo la 4
Mashahidi wa Yehova

(1) Mashahidi wa Yehova wanafikiri nini kuhusiana na makanisa mengine?

Makanisa mengine yote ni ya Kishetani.

(2) Mashahidi wa Yehova wanaamini kwamba mtu anapaswa afanye nini ili aokoke?

Ajiunge na taasisi yao, ajifunze mafundisho yao, na aanze kutendea kazi matakwa yao.

(3) Mashahidi wa Yehova wanaamini ninin kuhusu Roho Mtakatifu?

Roho Mtakatifu sio Mungu, lakini ni nguvu isiyo ya kinafsi ambayo inatoka kwa Mungu.

(4) Ni imani gani potofu inayofundishwa na Mashahidi wa Yehova kuhusiana na Yesu?

Yesu ni kitu cha kwanza kuumbwa na Mungu na alikuwa tu mtu mkamilifu, sio Mungu.

Somo la 5
Iglesia ni Cristo

(1) Maana ya jina Iglesia ni Cristo?

Kanisa la Kristo

(2) Imani muhimu sana ya Iglesia ni Cristo?

Ni kanisa la kweli, lililorejeshwa na Felix Manalo.

(3) Iglesia ni Cristo wanafundisha nini kuhusu Yesu?

Yesu alikuwa mtu maalumu lakini hakuwa Mungu.

(4) Kulingana na Iglesia ni Cristo, ni mambo gani mawili ambayo mtu anapaswa afanye ili aokoke?

Ajiunge na kanisa na kushika matakwa ya kanisa.

(5) Ni imani gani kubwa potofu ambayo inafanana na Iglesia ni Cristo katika mafundisho?

Mashahidi wa Yehova

Somo la 6
Eastern Lightning (Mwangaza wa Mashariki)

(1) Jina rasmi la Imani Potofu inayoitwa Eastern Lightning ni nini?

Kanisa la Mungu Mwenyezi.

(2) Eastern Lightning wanafundisha nini kuhusu Yesu?

- Jina la Yesu limepitwa na wakati na halina nguvu.
- Deng ndiye kristo kwa sasa.

(3) Kulingana na Eastern Lightning, mtu anapaswa afanye nini ili aokokewe?

Kuachana na Imani yake kwa Yesu na badala yake amfuate Deng, Kristo mwanamke.

Somo la 7
Imani Potofu za Kiapokaliptiki

(1) Ni kwa namna gani Imani Potofu za Kiapokaliptiki zinajaribu kukutana na hisia na mahitaji ya watu wa kiroho?

Kwa kuelezea hali ya ulimwengu na kile ambacho tunatakiwa kufanya ili kujiandaa.

(2) Ni kwa namna gani Imani Potofu za Kiapokaliptiki hutumia Biblia vibaya?

Wanasema kwamba Biblia inafundisha dhana zao, lakini kimsingi hutegemea mafunuo yao na huongeza maana kwenye Biblia ambayo hakiuwepo hapo kabla.

(3) Ni kwa namna gani nne ambazo Imani Potofu za Kiapokaliptiki ni haribifu?

- Huwavuta watu kutoka Makanisa ya Kikristo kuja katika mafundisho ya uongo.
- Huwavunja moyo washirika wao na kuwasababisha kupoteza Imani kabisa.
- Hudai kuwa Wakristo, lakini huwa na tabia zisizo za kikristo ambazo huharibu sifa ya Ukristo.
- Husababisha watu kutilia shaka maandiko kuhusiana na ufalme wa Mungu na Ujio wa Kristo.

(4) Dhana kuu ya maandiko ya kinaabii ni nini kutokana na Maandiko?

Mungu anatawala na hatimaye ataanzisha ufalme wake na kuwalipa wenye haki.

Somo la 8
Uhindu

(1) Ni kwa namna gani maadili ya miungu ya Uhindu inatofautiana na maadili ya Mungu mmoja wa kweli?

Miungu ya Uhindu wanatenda vyote viwili ubaya na wema.

(2) Brahman ni nini kulingana na Uhindu?

Nafsi au kitu muhimu katika kila kitu kinachoishi

(3) Ni nini dhana ya Uhindu kuhusu Yesu?

Baadhi ya Wahindu wanaamini kwamba Yesu alikuwa mtu ambaye alitendea kazi kanuni za Uhindu na alikuwa mwalimu mkuu. Hawaamini kwamba Yeye ni mwana pekee wa Mungu

(4) Lengo kuu la Uhindu ni kutafuta nini?

Ni kutafuta kuachiliwa kutoka katika mzunguko wa kuzaliwa tena na tena katika hali ya milele inayoitwa nirvana

Somo la 9
Ubudha

(1) Wabudha wanaamini nini badala ya Mungu?

Uhalisia mkuu ambao ni jumla ya kila kitu kinachoishi.

(2) Taja na Ufafanue Lengo kuu ka Mbudha?

Lengo kuu la Mbudha ni nirvana, ambayo inamaanisha hali ya kutokuwa chochote, mwisho wa nafsi.

(3) Wabudha wanatoa mafafanuzi gani kuhusiana na mateso katika maisha?

Mateso ni matokeo ya matamanio?

(4) Kwa nini Wabudha wanafanya mazoezi ya kiakili na ya kiroho?

Ili kumsaidia mtu kutoka katika ubinafsi.

Somo la 10
Utao

(1) Watao wanamuomba nani?

Miungu, roho, na mababu.

(2) Miungu wakuu wawili katika Utaoni nani?

- Yu-huang (Jade Emperor) ambaye anatawala juu ya miungu mingine na roho zote.
- Yuan-shih T'ien-tsun (kanuni kuu ya Kwanza) ana sifa za Mungu lakini hajihusishi na ulimwengu.

(3) Lengo la Mtao ni nini?

Ni kujileta mwenyewe katika usawa na nguvu katika ulimwengu. Lengo lake ni kuboresha afya yake na kurefusha maisha yake.

(4) Kulingana na Utao, Yesu ni nani?

Mtu ambaye ameendelea kiroho na ameonesha njia ya watu kuwa miungu.

Somo la 11
Uislamu

(1) Taja mungu, nabii, na kitabu kitakatifu cha Uislamu.

- Mungu: Allah
- Nabii: Muhammad
- Kitabu Kitakatifu: Qur'an

(2) Kweli nne kuhusu Yesu ambazo Waislamu wanazikataa?

- Alikufa msalabani.
- Alikuwa mwana wa Mungu.
- Ni Mungu aliyevaa mwili.
- Ni Mwokozi wa ulimwengu.

(3) Waislamu wanaamini nini kuhusu Biblia?

Biblia ilitoka kwa Mungu, lakini wanaamini kwamba kama kuna mgongano kati ya Biblia na kitabu chao kitakatifu Qur'an.

(4) Waislamu wanaamini nini kuhusu Biblia?

Wokovu unapatikana kwa kutimiza matakwa fulani yanayoitwa nguzo tano za Uislamu.

Somo la 12
Uyudaizimu

(1) Ni maandiko gani ambayo wote Wayudaizim na Wakristo wanayo?

Uyudaizimu na Ukristo wote unaamini Agano la Kale la Maandiko.

(2) Dhana ya wokovu kwa Uyudaizimu ikoje?

Wokovu unamaanisha kuokolewa katika hali ya uonevu au hali ambazo zinawazuia kumtumikia Mungu kama wanavyopaswa.

(3) Yesu alikuwa nani, kulingana na Uyudaizimu?

Yesu alikuwa mwalimu mwenye utata ambaye hakuwa Masihi wala Mungu.

(4) Uyudaizimu unamsuburi Masihi wa Aina gani?

Wanaamini kuwa Masihi hatakuwa Mungu aliyefanyika mwili, isipokuwa mtu maalumu aliyepakwa mafuta, atakayeleta amani katika ulimwengu.

Somo la 13
Dini ya New Age.

(1) Ni kwa namna gani wafuasi wa New Age wanaingiliana au kuwasiliana na ulimwengu wa roho?

Kwa kutumia namna yote ya Uchawi.

(2) Ni kwa namna gani wafuasi wa dini ya New Age hutazama dini nyingine?

Wafuasi wa New Age huweza kuvumilia kundi lolote la dini isipokuwa wale ambao hudai kuwa na kweli ambayo kila mtu ni lazima aamini.

(3) Dhana ya dini New Age kuhusu Mungu ni nini?

Dhana Mungu kwa wafuasi wa New Age ni ya kuwa kila kitu kwa pamoja ni Mungu

(4) Wafuasi wa New Age wanaamini nini kuhusu Yesu?

Yesu alikuwa mwanadamu ambaye alifahamu kutumia nguvu maalumu na alijaribu kuwafundisha wengine vivyo hivyo.

(5) Wafuasi wa New Age wanaamini nini kuhusu dhambi?

Wafuasi wa New Age hawaamini katika ukweli kuhusu dhambi, kwa sababu hawaamini katika Mungu alieweka viwango na waamuzi.

(6) Wafuasi wa New Age wanaamini nini kuhusu Wokovu?

Wafuasi New Age wanakataa dhana ya kibiblia ya wokovu na wanaamini kwamba suluhisho la matatizo ya wanadamu ni kukuza uelewa na nguvu za kiroho.

Somo la 14
Dini za Asili

(1) Je, imani na desturi za dini za asili zimejikita katika dini moja mahususi? Elezea.

Hapana. Imani nyingi na matendo ya dini za asili yanaweza pia kupatikana miongozi mwa waabudu wa dini nyine kubwa ulimwenguni ikiwemo Uhindu, Ubudha, Uvoodoo, na Uromani katoliki.

(2) Ni kwa jinsi gani wale wanaojishughulisha na dini za asili wanawasiliana na kuingiliana na maroho?

Kwa kutumia maneno, vitu, au matendo maalumu.

(3) Ushirikina ni nini?

Ushirikina ni dhana kwamba mtu anapaswa afuate matendo fulani kwa sababu vitu, matendo, au mahali fulani pana nguvu za kiroho.

(4) Kwa nini Wakristo sio washirikina?

Kwa sababu wanaamini nguvu kuu ya Mungu.

(5) Kwa nini Waabudu mizimu hawanuombi Mungu?

Kwa sababu wanafikiria kwamba haiwezekani kuhusiana Naye.

Somo la 15
Voodoo

(1) Wanaojishughulisha na Voodoo wanaabudu nini?

Shetani na roho chafu.

(2) Ni kutoka kwa dini gani dini ya Voodoo imeazima taratibu za ibada, sanamu na picha, na majina ya watakatifu?

Kanisa la Romani Katoliki.

(3) Lengo la anayeabudu katika ibada za Voodoo ni nini?

Kupagawa na roho

(4) Ni vitu gani hutumiwa wakati wa sherehe za ibada za Voodoo?

- Sadaka za Wanyama
- Kucheza
- Nyimbo
- Maombi
- Chakula
- Kuchora Michoro
- Nyoka
- Nguo Nyeupe
- Kupaka uso rangi

Somo la 16
Kuelewa Usabato

(1) Dhana ya Wasabato kuhusu Mungu ni nini?

Wasabato wanaamini katika Utatu, na Uungu wa Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu.

(2) Dhana ya Wasabato kuhusu wokovu ni nini?

Wokovu kwa njia ya Imani, na si kwa matendo.

(3) Wasabato wanaamini nini kitatokea kwa watu katika ufufuo?

Wakati wa ufufuo, wale waliokolewa watapokea uzima wa milele. Wale ambao hajaokolewa watafufuliwa kwa ajili ya hukumu na kisha kuharibiwa katika ziwa la moto.

(4) Wasabato wanajulikana kwa fundisho lao gani?

Fundisho lao la Sabato. Wanaamini kwamba Jumamosi, siku ya saba ya wiki, ndio siku sahihi kwa ajili ya Wakristo kupumzika na kuabudu.

Somo la 17
Kuelewa Uromani Katoliki

(1) Waromani Katoliki wanadai nini kutokana na jina lao?

Kuwa kanisa kamili la Mungu.

(2) Waromani Katoliki wanaamini nini kuhusu Mungu?

Waromani Katoliki wanaamini Utatu, uungu, kifo, kuzikwa, na ufufuo wa mwili wa Kristo na katika uungu wa Roho Mtakatifu.

(3) Kwa nini Waromani Katoliki wanashutumiwa kwa kuabudu sanamu?

Kwa sababu wanawaomba watakatifu kwa kutumia picha na sanamu zao

(4) Dhana ya Uromani Katoliki kuhusu wokovu ni nini?

Wokovu hautegemei tu upatanisho wa Kristo bali kwa kuwa sehemu ya kanisa Katoliki kupokea ushirika, na kutenda matendo mema.

(5) Fundisho la Toharani la Uromani Katoliki ni nini?

Baada ya kifo mtu anapaswa kutumikia adhabu ya dhambi kabla ya kuingia mbinguni.

Somo la 18
Kuelewa Uorthodoxy wa Mashariki

(1) Kanisa la Uorthodoxy wa Mashariki linadai nini?

Kwamba ndilo kanisa la kweli wakiwa na mafundisho na matendo ambayo yanatoa mwanga wa kumuabudu Mungu kwa usahihi.

(2) Kanisa la Uorthodoxy wa Mashariki linafundisha nini kuhusu Mungu?

Makanisa ya Uorthodoxy wa Mashariki yanaamini Utatu na uungu wa Kristo na Roho Mtakatifu.

(3) Kanisa la Uorthodoxy wa Mashariki linafundisha nini kuhusu Biblia?

Wanafundisha kwamba Biblia ni mamlaka ya mwisho kwa mafundisho yao, lakini ni lazima Biblia itafsiriwe na kanisa.

(4) Kwa nini wafuasi wa Uorthodoxy wa Mashariki wanaomba kwa watakatifu?

Wafuasi wengi wa Uorthodox wanamchukulia Mungu, na hata Yesu, kwamba yuko mbali na hajihusishi kuhusu wao.

(5) Kulingana na mafundisho ya Uorthodoxy wa Mashariki nini kinatokea katika *theosis?*

Katika *theosis* mwamini anabadilishwa pole pole na kuwa kama Mungu, anakuwa na asili ile ile ya utakatifu kamilifu.

Somo la 19
Kuelewa Theolojia ya Mafanikio

(1) Taja tabia nne zinazofanana za waalimu wa mafanikio ya uongo.

- Huwavuta waamini katika malengo ya kidunia badala ya kuwaitwa ili watubu.
- Hawatoi mtazamo halisi wa Kikristo juu ya mateso ya wanadamu.
- Wana mtazamo wa kiburi ambao hauheshimu makanisa mengine, wakristo wazee, na hata Mungu.
- Wanatoa ahadi ambazo Mungu hajazitoa, hupelekea watu kuvunjika moyo na kupoteza imani.

(2) Kulingana na theolojia ya mafanikio ya uongo, imani ni nini?

Nguvu fulani isiyo ya kinafsi na kiini cha ulimwengu

(3) Kulingana na theolojia ya mafanikio ya uongo, Mungu ni nani?

Mtu mwenye mwili.

(4) Kulingana na theolojia ya mafanikio ya uongo, watu ni nani?

Nakala za kifizikia za Mungu.